

# \*Wafugaji wajengewa uelewa wa Bima\*

NA STEPHANO MANGO,  
SONGEA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania, wametoa mafunzo ya Bima kwa Vikundi vya wakulima na Wafugaji wa Mkoa wa Ruvuma.

Akizungumza katika uzinduzi wa Mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji Jeremia Sendoro alisema, mafunzo hayo yameletwa Mkoa wa Ruvuma kwasababu, ni Mkoa wa kilimo na ufugaji wa Samaki kwa Wingi na wameona umuhimu wa kutoa Elimu na kuwajengea uelewa.

"Bima ya kilimo na Ufugaji inatusaidia pale tunapopata hasara katika mazao yanapokuwa

shambani, kama utatokea ukame au mvua za mawe pamoja na mifugo kufa kwa magonjwa au wanapokuwa malishoni bima inatoa fidia".

Sendoro, alitoa rai kwa wakulima na wafugaji kufuatia mafunzo hayo kufuata yale waliyopata kutoka kwa wataalamu na kuyafanyia kazi pamoja na kuwa na kilimo chenye tija na kuwa mabalozi kwa wengine ili kuepuka hasara katika kilimo na Ufugaji.

"Kuna wenzetu wa Bodi ya Kilimo, nafaka na mazao mchanganyiko Soya na mazao mengine katika mikataba yao walitaka Bima ya Kilimo utekelezaji ulikuwa mgumu kwasababu ya kukosa Bima".

Hata hivyo, alisema Mamlaka

ya Usimamizi wa Bima Tanzania wemekuwa wakati mzuri wa mavuno ikiwemo Soya, Maharagwe, Mahindi na Oktoba ni mwezi wa mavuno ya Korosho pamoja na Novemba kuandaa mashamba hivyo, mafunzo hayo yalitolewa wakati sahihi na kwa watakaopenda kilimo cha mkatiba na pamoja wataalamu watasimamia kilimo hicho.

Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) Kanda ya Nyanda za Kusini Salum Yungwa alisema, lengo la Mafunzo hayo Mkoani Ruvuma kutoa Elimu ya Bima ya Kilimo kwa wakulima ambao wanaoathirika na majanga mbalimbali yanayoweza kutokea wakati mazao yakiwa shambani, njiani au kwenye ghala.

NA  
KI

WA  
Min  
Wil  
na k  
bili  
wa r

F  
jini  
Maj  
jini  
Kan  
mrac

N  
ya k  
huo,  
tuni  
kilik  
tai